# Huduma za Afya ya Umma katika Kanda ya Kati

nova scotia health
Public Health
Central Zone

Afya ya Umma inatoa huduma na rasilimali zinazokuza afya na kuzuia kuenea kwa magonjwa katika jamii zetu. Huduma zetu huanza kabla ya kuzaliwa na kuendelea katika maisha yako yote. Huduma hutolewa majumbani, mashuleni, jamii na Ofisi ya Afya ya Umma huko Dartmouth. **Huduma zote ni bure na wakalimani wanapatikana.**

**Wasiliana nasi:**

902-481-5800

www.nshealth.ca/Public-Health




## Huduma Mashuleni

### Programu ya Kupaka Fluoride

Fluoride ni madini salama, ya asili ambayo husaidia kufanya meno kuwa na nguvu na kuzuia mashimo. Afya ya Umma inatoa programu ya kupaka Fluoride bila malipo katika baadhi ya shule za msingi ili kusaidia kuzuia kuoza kwa meno ya watoto. Katika programu hii, Mtaalamu wa Usafi wa meno hupaka fluoride kwenye meno ya wanafunzi. Ikiwa mtoto wako yuko kwenye shule yenye programu hii, mwalimu wao atakupa taarifa zaidi.

**902-481-5800 ext. 4** **www.nshealth.ca/PHOralHealth**

### Programu ya Chanjo Shuleni

Afya ya Umma inafanya kazi pamoja na shule kutoa chanjo za bure, za kawaida kwa wanafunzi wa Darasa la 7 wakati wa mwaka wa shule. Ikiwa mwanafunzi atakosa chanjo, bado anaweza kupata bure hadi atakapofikisha miaka 19 kwa kupiga simu kwa Afya ya Umma ili kuweka miadi.

**902-481-4956** **www.nshealth.ca/school-immunization-program**

### Vituo vya Afya ya Vijana

Vituo vya Afya ya Vijana (YHC) ni maeneo salama, ya kukaribisha na ya kuunga mkono ambapo wanafunzi wanaweza kupata msaada wa kibinafsi kupitia mazungumzo ya siri na Mratibu wa Kituo cha Afya ya Vijana (YHCC). YHCC inaweza kutoa usaidizi wa afya ya akili, udhibiti wa mafadhaiko na jinsi ya kukabiliana, na kuwasaidia wanafunzi kupata usaidizi na huduma zingine shuleni, jumuiya au mfumo wa afya, ikihitajika.

YHCC pia inafanya kazi na vijana na viongozi wengine wa shule kusaidia mazingira mazuri ya shule na kuunda fursa za ustawi, kama vile vilabu vya shule na hafla.

YHC ziko katika shule zote za sekondari na baadhi ya shule za kati. Nenda YHC shuleni kwako ili kujifunza zaidi.

**902-481-5800** **www.nshealth.ca/health-promoting-schools**

*Agosti 2025*

# Huduma za Afya ya Umma katika Kanda ya Kati

nova scotia health
Public Health
Central Zone

**Huduma zote ni bure na wakalimani wanapatikana.**




## Huduma Majumbani na Jamii

### Miaka ya Mwanzoni

Unapoungana na Miaka ya Mwanzoni, Muuguzi wa Afya ya Umma atafanya kazi na familia yako kutoa usaidizi ambao utakidhi mahitaji yako vyema. Hii inaweza kujumuisha kusaidia ukuaji wenye afya na maendeleo ya mtoto wako, usaidizi wa kunyonyesha/kumlisha mtoto mchanga, usaidizi wa afya ya akili au kukuunganisha na huduma zingine za afya na jamii.

**902-481-4967** **www.nshealth.ca/Pregnancy-Supports | www.nshealth.ca/Parenting-Supports**

### Kliniki za Chanjo ya Watoto

Afya ya Umma inatoa Kliniki za Chanjo za utotoni katika ofisi yetu huko Dartmouth mara moja kwa wiki. Tunatoa chanjo za bure, za kawaida kwa watoto ambao hawana mtoa huduma ya msingi.

**902-481-4956** **www.nshealth.ca/public-health-immunization-clinics**

### Kitengo Cha Afya ya Umma kwa Kutumia Gari

Huduma hii kwa njia ya gari, inapelekwa kwenye jumuiya ili kutoa chanjo, vipimo, na uelekezaji wa huduma za afya. Mara nyingi hufanya kazi na mashirika kama vile YMCA na maktaba za karibu ili kutoa huduma za kliniki katika maeneo ambayo yanafahamika na karibu na nyumbani.

**www.nshealth.ca/PHMU**

### Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yanayoambukiza

Wakati ugonjwa wa kuambukiza unapotambuliwa, Afya ya Umma hufanya kazi na watu binafsi na washiriki wengine ili kupunguza kuenea katika jamii, pamoja na vituo vya kulelea watoto, mashuleni na mahali pa kazi. Afya ya Umma inaweza kutambua watu ambao wamekuwa karibu na mwathirika, kuwasiliana nao ili kutoa mwelekeo na kupanga vipimo na dawa.

**902-481-5824 (tafadhali acha ujumbe)** **www.nshealth.ca/infectious-diseases**

**Wasiliana na Afya ya Umma Kanda ya Kati:** **902-481-5800** **www.nshealth.ca/Public-Health**

*Kurasa za tovuti zinapatikana kwa Kiingereza tu*

*Agosti 2025*